



Bi kizee mmoja  
alikuwa na kuku na  
Jogoo mzee.




Mjukuu wake  
alimtembelea.  
Aliamua kumchinja  
yule Jogoo mzee.





Jogoo alitorokea  
jijini ili kujiokoa.



Njiani, Jogoo  
alimkuta Paka.  
Alikuwa akitoroka  
kutoka kwa  
mkubwa wake.





Jogoo na Paka  
walimkuta Mbwa  
akitoroka pia.



Farasi aliyekuwa  
akitoroka, alijiunga  
nao.





Wanyama hao  
waliwaona wezi  
ndani ya nyumba.



Walitaka  
kuwafukuza wale  
wezi. Waliimba kwa  
sauti ya juu.





Wezi walitoroka.  
Wanyama walikula  
chakula chote  
walichopata mle  
nyumbani.



Wezi waliamua  
kurudi baadaye.  
Lakini, wanyama  
waliwavamia.





Wezi walitoroka  
wakaenda zao  
kabisa.



Wanyama waliishi  
pamoja katika  
nyumba ile kwa  
furaha.